

Utohozi kama Mkakati wa Mawasiliano katika Mazungumzo kuhusu Ukimwi katika Ekegusii

Carren Nyandiba
Chuo Kikuu cha Rongo, Kenya

Ikisiri

Tangu kisa cha kwanza cha ukimwi kugunduliwa nchini Kenya, juhudi mbalimbali zimefanywa kujaribu kupunguza idadi ya visa vya maambukizi mapya. Juhudi hizo ni pamoja na kuelimisha umma kuhusu mbinu na njia mbalimbali za kujikinga dhidi ya maambuki. Elimu kuhusu Virusi vya ukimwi (VVU) na ukimwi hutolewa kwa lugha mbalimbali kutegemea hadhira lengwa. Tafiti zimefanywa kuhusu umuhimu wa lugha katika mawasiliano mbalimbali yakiwemo mawasiliano kuhusu ukimwi. Mawasiliano kuhusu VVU/ukimwi husheheni mijadala kuhusu sehemu za siri, kitendo cha ngono, matumizi ya kondomu na watu wanaoishi na VVU miongoni mwa mambo mengine. Ingawa mawasiliano ya aina hiyo hufanyika kwa lugha wazi katika Kiingereza, tafiti zimeonyesha kwamba masuala hayo ni mwiko katika baadhi ya lugha za Kiafrika na kwa hivyo hayawezi kujadiliwa kwa lugha wazi. Makala haya yanachunguza utohozi unavyotumka katika mijadala kuhusu VVU/Ukimwi katika lugha ya Ekegusii. Mjadala ambao unajitokeza katika makala haya ulichochea na sababu kwamba Ekegusii ni mojawapo ya lugha ambazo zimeweka mwiko kwa mazungumzo kuhusu mambo hayo. Aidha, utafiti ulitaka kuchunguza namna lugha ya Ekegusii inakabiliana na suala ambalo limeibuka katika jamii ya sasa. Lengo la Makala haya ni kujadili namna utohozi umetumika katika kujadili sehemu za siri, kitendo cha ngono na matumizi ya kondomu katika diskosi za VVU/Ukimwi.

Maneno Muhimu: Utohozi, Mawasiliano, Ukimwi, Ekegusi

Utangulizi

Janga la ukimwi ni suala ambalo linashughulisha serikali, mashirika yasiyokuwa ya serikali, wataalamu wa afya na wananchi kwa jumla katika mataifa mengi ya ulimwengu likiwemo taifa la Kenya. Mikakati mbalimbali imewekwa ili kuweza kupunguza maambukizi mapya na pia kutoa huduma kwa watu wanaoishi na virusi.

Mojawapo ya mikakati hiyo ni upimaji wa hiari wa wanajamii ili kutambua hali zao za VVU. Upimaji huo wa hiari huambatana na nasaha kuhusu masuala mbalimbali.

Utoaji wa nasaha na upimaji wa kujua hali ya maambukizi hufanywa katika vituo vya Upimaji na unasihi wa Hiari (UUH). Kote ulimwenguni, vituo hivi vimetokea kuwa njia isiyokuwa na gharama kubwa katika kupunguza maambukizi ya VVU/ukimwi, (Ambasa –Shisanya, 2009). Kwa kutembelea vituo vya UUH, watu wanaotaka kujua hali zao huweza kuzijua. Vituo vya UUH hutoa ushauri na nasaha kwa watu katika kuelewa mambo muhimu kuhusu hali ya VVU/Ukimwi na kufanya uamuzi wa kupimwa au kutopimwa. Brown na wenzake (2001) wanasema kwamba huduma za UUH hutolewa kulingana na sheria kwamba kila mtu ana haki ya kujua au kutojua hali yake ya VVU. Malengo mahsusi huduma za UUH ni:

- i) Kugundua hali ya mhusika mapema;
- ii) Kuwaelimisha walioambukizwa wajiepushe kueneza virusi kwa wengine kimaksudi;
- iii) Kuwasaidia walioambukizwa kutunza hali zao za afya kwa kubadili mienendo yao;
- iv) Kuwasaidia walioambukizwa kufanya maamuzi kuhusu maisha yao;
- v) Kusaidia walioambukizwa kufanya uamuzi kuhusu iwapo wangependa kuzaa watoto na jinsi ya kupunguza uwezekano wa kuwaambukiza watoto hao kabla ya kuzaliwa.

Mawasiliano kuhusu VVU/UKIMWI hushehania mijadala kuhusu ngono na kujamiiiana, sehemu za siri na matumizi ya kondomu, masuala ambayo ni nyeti katika jamii nyingi (Sorcar, 2009). Kwa hivyo, uchunguzi wa lugha na miktadha ya kimawasiliano inayolenga tamaduni za wanajamii ni muhimu sana katika vita dhidi ya VVU/UKIMWI (Airhihenbuwa na Obergon, 2000). Wataalamu mbalimbali wamefanya tafiti kuhusu lugha na VVU/UKIMWI. Miongoni mwa wataalam hao ni (Jones, 1996; Moto, 2004; Ogechi, 2006; Kobia, 2008; Veliswa, 2009; Sorcar, 2009; Nyandiba, 2013).

Sorcar (2009) anadai kwamba kuelimisha watu kuhusu VVU/UKIMWI ni jambo gumu kwa sababu hali ya VVU huhusishwa na masuala nyeti kama vile ngono, matumizi ya kondomu, uasherati, ndoa za jinsia moja na kadhalika. Haya yote ni masuala ambayo yamewekewa mwiko wa kiisimu na kitamaduni katika jamii nyingi za ulimwenguni. Kwa hivyo mawasiliano kuhusu masuala hayo nyeti ‘hugeuzwa’ ili kuingiliana na kaida za tamaduni jamiilugha husika (Sorcar, keshatajwa). Tafiti zimeonyesha jinsi wanajamii tofauti wanatumia mbinu na njia mbalimbali za kujadili suala la VVU/ukimwi. Baadhi ya mbinu zinazotumika katika mijadala hiyo ni mafumbo, tasfida, uchanganyaji msimbo na pia utohozi (Moto, 2004; Ogechi, 2007; Kobia, 2008).

Katika utafiti unaohusu vipengee mbalimbali vya lugha, haitoshi tu kujua lugha ya watu, au kuelewa baadhi tu ya maadili ya jamii fulani, bali ni muhimu pia kuelewa desturi na sheria za utamaduni zinazoathiri maingiliano ya watu, yawe ya siri au ya

hadharani. Mazungumzo na elimu ya ushauri kuhusu ukimwi yanayotolewa na washauri katika hospitali na vituo vya ushauri hufanyika hadharani na yanahusu mijadala kuhusu ngono, VVU na ukimwi na yanapaswa kutolewa kwa lugha wazi. Washauri wa UUH hawana budi kutekeleza majukumu yao huku wakitilia maanani miktadha ya kitamaduni-jamii na lugha mwafaka (Iwuagwu 2003).

Huduma za UUH na mijadala kuhusu VVU/UKIMWI hazipatikani tu hospitalini bali hutolewa pia katika vituo mahususi vilivyoko katika maeneo mbalimbali katika jamii. Pia, utafiti huu uligundua kwamba mijadala kuhusu VVU/UKIMWI hufanyika kanisani (katika vipindi maalum), redioni, katika mabaraza ya machifu na hata katika mazungumzo ya hadharani miongoni mwa wanajamii. Katika hali hii, ni kana kwamba ushauri unaweza kutolewa na kila aina ya mtaalamu, almradi anaweza kuwasiliana na kuelekeza mabadiliko ya kitabia. Hata hivyo, iwapo mafunzo yatatolewa kwa njia na lugha mwafaka, ujumbe utaeleweka ipasavyo na mawasiliano hayo yatakuwa na umuhimu, lakini yakifanyika kwa lugha isiyofaa, huenda ujumbe ukapotoka ama kutoeleweka kabisa (Veliswa, 2009). Makala haya yanalenga kujadili utohozi kama mkakati wa mawasiliano unaotumiwa na wahudumu wa hospitali wanapotoa nasaha kuhusu VVU/ukimwi katika lugha ya Ekegusii. Aidha ulichunguza namna mbinu hiyo ilitumika kujadili masuala ya sehemu za siri, kitendo cha ngono na matumizi ya kondomu katika mijadala iliyotokea katika maeneo mbalimbali ya kimawasiliano ilmradi yalifanywa kwa lugha ya Ekegusii.

Mbinu za Utafiti

Utafiti kwa minajili ya makala haya ulifanywa kwa kurekodi mazungumzo ya nasaha na ushauri yaliyotolewa katika hospitali na vituo vinavyotoa huduma za VVU/ukimwi katika eneo la Kisii. Mazungumzo yaliyolengwa ni yale yaliyofanyika kwa lugha ya Ekegusii na wala si yale yaliyofanyika kwa Kiswahili ama Kiingereza. Aidha mazungumzo ya ushauri na nasaha yanayotolewa katika vipindi mbalimbali vya redio zinazotangaza kwa lugha ya Ekegusii yalirekodiwa na kutumika katika upataji wa data. Mazungumzo katika vipindi maalum kanisani vinavyolenga kutoa nasaha kuhusu VVU/ukimwi pia yalitumika katika kuzoa data kwa minajili ya makala haya. Data nyingine ilipatikana kwa kusikiliza na kurekodi mazungumzo ya hadharani ya wanajamii katika miktadha mbalimbali pamoja na kusikiliza nyimbo za Ekegusii zinazoangazia ugonjwa wa Ukimwi.

EkeGusii

Ekegusii ni lugha ya Kibantu inayozungumzwa na jamii mojawapo ya Wabantu wa Mashariki mwa Nyanza. Ni lugha iliyo katika jamii moja na lugha za Kuria, Ngurimi, Zanaki, Shashi na Ikuzi (Nurse na Phillipson 1980). Kwa sababu ya wazungumzaji wa Ekegusii kupakana na wanailoti kama vile Wakipsigis, Wamaasai na Waluo, lugha hii inasheheni msamiati mwingi wa kukopa (Nyakoe, 2011). Ongarora (1995) anadai kwamba lugha hii ina lahaja mbili kuu, Ekerogoro na Ekemaate. Abagusii wanaongozwa na sheria zinazoitwa **chinsoni** (sheria za heshima), zinazowazuia kutenda au kusema jambo la aibu hadharani, Akama na Maxon (2006). Kwa sababu

hiyo, lugha hii imejaa tasfida, mafumbo na utohozi. Aidha, lugha ya EkeGusii ina lugha mwiko (Nyakoe, 2011) ambapo baadhi ya masuala ambayo ni mwiko katika lugha hii ni pamoja na ngono, sehemu za mwili zilizofichika, haja za kibaolojia na matusi. Utohozi ni mojawapo ya mbinu za kuingiza maneno mapya katika lugha na kwa njia hiyo kuongezea msamiati wa lugha (Mweri, 2010). Maneno ambayo hutoholewa ni yale ya vitu ama dhana ambazo kiasili hazikuwepo katika jamii hii ama iwapo vilikuwepo, vimepata maneno mengine mapya ya kuvirejelea. Makala haya yanachanganua utohozi ulivyotumika katika kujadili VVU/ukimwi, sehemu za siri za wanawake na wanaume na kondomu kama kifaa cha kuzuia maambukizi.

Utohozi kama Mkakati wa Mawasiliano

Utafiti huu ulichunguza jinsi utohozi ulivyojitokeza katika mazungumzo kuhusu VVU/ukimwi. Kulingana na Kamusi kuu ya Kiswahili (2017) utohozi ni hali ya kufanya matamshi au maandishi ya neno fulani la kigeni yalingane na matamshi au maandishi ya lugha nyingine. Utohozi unarejelea mabadiliko ya kimuundo na kimsamiati yanayotokea katika lugha ili kutimiza mahitaji kimatumizi ya lugha hiyo (Coulmas, 2005). Mtaalam huyu anaendelea kudai kwamba lugha ni mfumo unaobadilika kadri jamii inavyobadilika. Lugha mbalimbali kama vile Kiarabu, Kiswahili, Kijerumani, Kihebrania na nyinginezo zimeweza kudhihirisha utohozi. Mugambi (2012) anaeleza kwamba mbinu za utohozi katika lugha ni pamoja na usogezi maana, upanuzi maana, ufinyizi maana, tasfida na uimarikaji maana. Utohozi katika lugha huweza kuwa na ruwaza mbalimbali.

Mahitaji ya lugha ndiyo huchangia katika kuwepo kwa utohozi. Lugha hukua na kupanuka kupitia kwa utohozi (Coulmas, 1989; Mugambi, 2012) Utafiti huu ulichunguza utohozi katika lugha ya Ekegusii. Uchunguzi huu ulijikita katika utohozi wa msamiati ulijitokeza katika mazungumzo kuhusu VVU/UKIMWI. Utafiti huu ulihakiki maneno yaliyotoholewa kwa kuchunguza lugha asilia ya neno na kisha kueleza mbinu iliyotumika katika utohozi wa neno hilo. Jedwali la 1 linaonyesha mifano ya maneno yaliyotoholewa, maana zao na lugha asilia ya maneno hayo. Jumla ya maneno 15 yalikuwa yametoholewa ambapo 7 kati ya hayo yalitoholewa kutoka kwa Kiingereza, na 8 yakatoholewa kutoka kwa Kiswahili.

Jedwali 1: Mifano ya Utohozi kuhusu VVU/UKIMWI na Sehemu Za siri

Neno	Lugha asilia	Neno asilia	Maana
Ebirusi	Ks	Virusi	Vvu
okimwi	Ks	Ukimwi	Ukimwi
ekondomu	Kn	<i>Condom</i>	kondomu
Esidi	Kn	<i>Cd</i>	kondomu
egabana	Kn	<i>Governor</i>	kondomu
Esogisi	Kn	<i>Socks</i>	kondomu
Egesima	Kn	Kisima	Kuma
Ekaramu	Ks	Kalamu	Mboo
Epensiri	Kn	<i>Pencil</i>	Mboo

Egetabu	Ks	Kitabu	Kuma
Ekobia	Ks	Kofia	Kondomu
Ebuti	Kn	<i>Gumboots</i>	Kondomu
Esaba	Kn	<i>Server</i>	Kuma
Egatiba	Ks	Katiba	Ngono
Parepare	Ks	Palepale	Kuma
Jumla/asilimia	15=100		
Jumla/asilimia	Kn 8=53		
Jumla/asilimia	Ks 7=47		

Kutokana na mifano hii, tunaona kwamba maneno 8 yaliyotoholewa yalikuwa ya asili ya Kiingereza. Hii inachangia asilimia 53 ya maneno yote yaliyotoholewa, nayo maneno 7 yaliyotoholewa yalikuwa ya asili ya Kiswahili. Utohozi wa maneno ya Kiswahili ulichangia asilimia 47. Maneno ya Kiswahili, “virusi” na “ukimwi” yametoholewa na kufanywa ya Ekegusii, na yakawa **ebirusi** na **okimwi** mtawalia. Yalipoingizwa katika lugha ya Ekegusii, yaliwekwa katika ngeli mbalimbali, kwa hivyo yaliongezewa viambishi awali vinavyotambulisha ngeli ambapo yaliingizwa. Baadhi ya maneno hayo yaliingia katika ngeli ya *e- chi*, kwa mfano:

esogisi	chisogisi
egabana	chigabana
esidi	chisidi
ekondomu	chikondomu
egatiba	chigatiba
esaba	chisaba

Lengo la utafiti huu si kuonyesha ngeli ya nonino au miundo ya maneno yaliyotoholewa, bali ni kuonyesha mbinu zilizotumika katika utohozi. Mbinu zilizotumika katika utohozi wa maneno ni upanuzi wa maana, uhamishaji, ufupi na tasfida.

Utohozi kutokana na Upanuzi wa Maana

Utafiti huu uligundua kwamba utohozi ulifanyika kwa kupanua maana ya kawaida ya dhana au kitu fulani. Kwa mfano, katika hali ya kawaida, **egabana** (*speedgoverner*) ni kidhibiti mwendo cha magari barabarani. Kifaa hiki kilianza kutumiwa katika magari ya usafiri wa umma nchini Kenya mnamo mwaka wa 2003 baada ya nchi kushuhudia idadi kubwa ya ajali za barabarani zilizotokana na kasi ya uendeshaji wa magari. Kwa hivyo wakati washauri wanarejelea kondomu kama **egabana**, maana ya kila siku ya kifaa hiki inapanuliwa. Kondomu inapewa jukumu la kudhibiti kasi ya virusi kutoka kwa mtu mmoja hadi mwingine. Kufanya ngono bila kondomu kunachukuliwa kama kuhatarisha maisha jinsi kuendesha gari kwa kasi barabarani kunavyofanya. Vivyo hivyo kutumia utohozi kunasaidia katika kupunguza aibu ambayo matumizi ya neno halisi ingeleta, na hilo ndilo lengo la uteuzi mwafaka wa maneno katika mawasiliano (Cain, 2011).

Mfano mwingine wa upanuzi wa maana kupitia kwa utohozi ni **ebuti-chibuti** (*gumboots*). Maana ya kawaida ya **chibuti** ni viatu vizito ambavyo huvaliwa hasa mtu anapotembea mahali penye tope au miiba ili kuepuka kukanyaga tope au kudungwa na miiba. Kuita kondomu **ebuti** kunatokana na kitendo cha ngono kufananishwa na kutembea kwenye matope au kwenye miiba. Katika ufananisho huu, sehemu ya siri ya mwanamke inamithilishwa na tope au miiba yenye kuhatarisha mguu (sehemu ya siri ya mwanaume). Kwa hivyo kuvaa **ebuti** kunakingamguu usikanyage tope au kudungwa na miiba jinsi kondomu inavyokinga wanaoshiriki ngono kutokana na maambukizi. Upanuzi unafanywa kwa kutumia vitu vya kawaida katika kujadili mada ambazo ni mwiko kujadiliwa kwa lugha wazi. Cain (2011) anadai kwamba washiriki hujaribu kuepuka aibu kwa kuteua maneno mwafaka ya kutumia katika mawasiliano. Aidha, yaelekea kwamba upanuzi katika kuzungumzia maswala ya ngono na VVU/ukimwi hujitokeza kama ilivyogunduliwa na watafiti wengine (Moto, 2004; Ogechi, 2006).

Utohozi kutokana na Uhamishaji Maana

Katika aina hii ya utohozi, maana ya kawaida ya neno inahamishwa na kutumika katika kuelezea hali nyingine. Katika utohozi kwa uhamishaji maana, kuna mifano ya **ekobia** (kofia), **esogisi** (*socks*), **ekaramu** (kalamu) na **ebensiri** (*pencil*). Maana ya kawaida ya **ekobia** (kofia) ni aina ya nguo inayovaliwa kichwani. Katika matumizi yake, maana hiyo inahamishwa na kupewa kondomu ambayo huvishwa uume ili kuzuia maambukizi ya VVU. Kwa hivyo, maana ya kawaida ya kichwa cha mtu inahamishwa na kupewa uume, ambao ndio huvishwa kondomu.

Kofia inapovaliwa hutekeleza majukumu kama vile kuzuia kichwa kisipigwe na jua kali, kujikinga na mvua na pia kama mojawapo ya mavazi ya watu. Kondomu inapopewa jina la **ekobia**, inapewa jukumu la kukinga au kuzuia maambukizi miongoni mwa watu wanaoshiriki ngono. Kwa hivyo, kuna hali ya uhamishaji wa maana ya kawaida ya **ekobia** kutoka kuwa nguo inayovaliwa kichwani na kuwa kondomu inayovishwa uume. Kwa upande wake, maana ya kawaida ya **esogisi** (soksi) ni aina ya nguo inayovaliwa miguuni kabla ya kuvaa viatu. Ulinganisho wa kondomu na soksi unaweza kuwa umetokana na kulinganisha kitendo cha kuvaa soksi na kile cha kuvaa kondomu. Wakati wa kuvaa soksi, mtu hunyoosha mguu wake na kuweka vidole vya mguu pamoja, kisha huiingiza kwa kuivuta juu. Hatua ya kuvaa kondomu inamithilishwa na ile ya kuvaa soksi na si ajabu kwa hivyo kwa kondomu kuitwa, **esogisi**. Ni muhimu kueleza kwamba kondomu iliyorejelewa kama **esogisi** ni ile ya wanaume wala si ya wanawake.

Mfano mwingine wa utohozi kwa upanuzi wa maana ni **esidi** au **esiti** (*CD*). Katika mfano huu, kitendo cha kuvaa kondomu kimemithilishwa na kitendo cha kuingiza *CD* kwenye mashine. Wakati wa kuingiza *CD*, mtu huisukuma ndani ya kidude ambacho kinaishikilia ili iweze kucheza. Utohozi huu wa kupanua maana ya kawaida ya **esidi** au **esiti** (*CD*) kunasaidia katika kupunguza aibu katika mawasiliano ya VVU/UKIMWI. Uepukaji au upunguzaji wa aibu ndilo lengo kuu lauteuzi mwafaka wa lugha ya kutumia katika mawasiliano (Cain, 2011).

Matumizi ya neno **esaba (server) kumaanisha** sehemu ya siri ya mwanamke ni mfano mwingine wa utohozi kwa kuhamisha maana. Dhana hii ilianza kutumika baada ya kesi ya matokeo ya urais nchini Kenya ambapo kulikuwa na tuhuma kwamba Kamisheni huru ya uchaguzi na mipaka almaarufu *Independent Electoral and Boundaries Commission (IEBC)* ilikataa kufungua seva ambapo matokeo ya uchaguzi wa tarehe 8/8/2017 yalikuwepo. Kwa mujibu wa Kiputiputi (2011) seva ni programu inayosimamia rasilmali za mtandao na kuzihudumia programu nyingine. Anaendelea kusema kwamba seva ya mtandao inasimamia data na taarifa zinazobaligishwa kwenye mtandao na seva ya hazinadata. Hali hiyo ya *IEBC* kukataa kufungua seva ndiyo ilimithilishwa na kupata ruhusa au kunyimwa ruhusa ya kufanya ngono. Neno **esaba** lilitumika muktadha ambapo wanaume walishauriwa kutumia kondomu baada ya kufunguliwa seva yaani sehemu ya siri ya mwanamke. Mfano ufuatao unadhihirisha hali hii:

1. **Muktadha:** Mazungumzo haya yalisikika katika kipindi cha redio (Egesa Fm) ambapo msemaji ambaye pia alitambuliwa kama mshauri wa afya aliwaambia wanaume watumie mpira baada ya kufunguliwa seva.

Msh: Aye buna omomura, ekero gwachorire emestari yao yonsi pi mbaka bwanchire gokoigorera esaba, inyora bono kobeka esogisi...

Wewe kama mvulana baada ya kuchora mistari yako yote hadi amekubali kukufungulia seva, kumbuka basi kuvaa soksi.

Katika mfano huu, neno *server* limetoholewa na kuwa **esaba** na kisha maana yake ikahamishwa na kutumika katika muktadha wa ngono la kurejelea sehemu ya siri ya mwanamke. Ingawa sehemu hiyo ina jina kamili linaloirejelea, ni mwiko kwa wanajamii hii kulitumia jina hilo katika mazungumzo ya hadharani, kwa hivyo mbinu mbali mbali hutumika katika kuepuka aibu katika mazungumzo.

Utohozi kutokana na tasfida

Tasfida inarejelea aina ya usemi ambapo msemaji hutumia lugha ya staha au ya kificho badala ya kutumia moja kwa moja lugha ya matusi au yenye kukera ikisemwa hadharani (Kamusi kuu ya Kiswahili, 2017). Kwa hivyo, tasfida ni matumizi ya tamathali za usemi kwa lengo la kuifanya lugha ipendeze na ikubalike katika utamaduni wa wasilikizaji. Kutumia tasfida katika mazungumzo ni kama kuivisha lugha mavazi mazuri ili kuifanya ipendeze (Wardhaugh, 1999). Katika mazungumzo ya kawaida, tasfida hutumika mahali pa maneno ambayo ni mwiko kutajwa. Tasfida huwawezesha wazungumzaji kuelezea mambo yasiyopendeza kwa njia ambayo inakubalika na hivyo kuondoa aibu kwa wasikilizaji. (Cain, 2011) unadai kwamba mazungumzo huongozwa na vipengee mbalimbali, ambapo mojawapo ya vipengee hivyo ni wahiji. Kwa hivyo, mazungumzo kwa vyovyote vile hulenga kuondoa aibu kwa wazungumzaji na wasikilizaji. Utohozi uliotokana na tasfida ndiyo njia mojawapo iliyotumiwa na washauri katika kuondoa aibu kwa wasikilizaji.

Mifano ya maneno yaliyotoholewa na ambayo yalitumika kama tasfida ni **egetabu** (kitabu), **egesima** (kisima) **egatiba**(katiba) na **esaba** (server). **Egetabu** limetoholewa

kutoka neno la Kiswahili, kitabu na maana yake ya kawaida ni datfari ambalo mtu huandika kwa kutumia kalamu. Mshauri alilinganisha sehemu ya siri ya mwanamke na kitabu nayo sehemu ya mwanaume inalinganishwa na kalamu au penseli. Kwa kawaida mtu anapotaka kuandika kitabu, inambidi afungue ukurasa na kisha kuanza kuandika. Kulinganisha sehemu ya mwanamke na kitabu na ya mwanaume kalamu ni njia mojawapo ya kuepuka aibu ya kutaja sehemu hizo kwa majina yake katika Ekegusii, yaani **embere** (kuma) na **embo** (mboo) katika mijadala kama hii iliyotolewa hadharani. Vilevile ulinganisho huo unatokana na kitendo cha kufanya ngono na kile cha kuandika. Hata hivyo utafiti huu uligundua kwamba ulinganisho wa sehemu hiyo na kitabu ulifanywa kwa lengo la kuhimiza hasa wanawake kuwa waaminifu kuhusiana na suala la ngono. Katika mfano nambari 1 mshauri katika mkutano mmojawapo mshauri alitoa tamko lililodhihirisha hali hiyo.

2. Muktadha: Mazungumzo haya yalitokea katika mkutano wa ushauri ambapo mshauri (msh) aliwaeleza wanawake wasifanye ngono kiholela, na akatumia utohozi wa neno **egetabu** kurejelea sehemu ya siri ya wanawake

Msh: **Aye buna omosubati mbwanche egetabu kiao kerikwe na karamu ende yonsi?**

Wewe kama mwanamke, unaweza kutaka kitabu chako kuandikwa kwa kalamu yoyote?

Tamko hili linawalenga wanawake kuliko wanaume, na ni kama onyo pia kwa wanawake. Ujumbe unaotokana na mfano huu ni kwamba mwanamke alihitajika alinde **egetabu** (uke wake) ili kisiweze kuandikwa na kalamu (uume) yoyote. Onyo hili linaonyesha kuwa katika kitendo cha ngono, mwanamke ana uwezo wa kuamua iwapo atashiriki na kwamba ni nani watafanya naye kitendo hicho.

Neno **egesima** limetoholewa kutoka kwa neno na Kiswahili, kisima. Kisima ni shimo ndefu inayochimbwa ardhini na ambayo huwa na maji yanayotekwa. Katika utekaji wa maji kutoka kisimani, mtu huhitaji ndoo au kibuyu anachoweza kutumbukiza ndani ya kiisima hicho na kuteka maji. Utekaji wa maji kutoka kisimani huhitaji makini, la sivyo maji huchafuka na hivyo hayawezi kuwafaa watumizi wake. **Egesima** limetumika kama tasfida ya kulinganisha sehemu ya siri ya mwanamke. Matumizi ya **egesima** yaliwalenga wanaume kama tamko katika mfano nambari 2 linadhihirisha.

3. Muktadha: Tamko hili lilitolewa na mshauri alipokuwa anatoa onyo hasa kwa wanaume kuwa waaminifu kwa washirika wao wa ngono.

Msh: **Mosacha onde bwensi ore aaga, manya ing'a ense yabeire bobee... kanyweamache y'egesima kiao.**

Mwanaume yeyote aliye hapa, ufahamu kuwa dunia imeharibika... kunywa maji ya kisima chako.

Lengo la ulinganisho huo ni kuonesha kwamba maji ya kisima ambacho watu wengi huteka huwa yamechafuka. Vivyohivyo, mwanaume anaambiwa aweze kuwa

mwaminifu kwa mwanamke mmoja, asiwe wa ‘kuteka maji katika visima mbalimbali’ (kufanya ngono na wanawake wengi). Kutokana na utohozi wa tasfida, masuala ya ngono yaliweza kujadiliwa bila kuleta aibu kwa msikilizaji yeyote, na hili ndilo lengo kuu la uteuzi mwafaka wa lugha katika mawasilaino (Cain, 2011).

Mfano mwingine wa utohozi kutokana na tasfida ni ule wa kutumia neno **egatiba** (katiba) kurejelea kitendo cha ngono. Kamusi kuu ya Kiswahili (2017) inafasili katiba kama mkusanyiko wa sharia na kanuni zinazotumiwa kuendesha shughuli za nchi, chama au kikundi au watu wenye malengo wenye malengo yanayofanana. Hata hivyo katika hali hii, neno hilo limetumika kama tasfida kuelezea kitendo cha ngono. Ingawa kitendo hicho kina neno la Ekegusii ambalo linapaswa kutumika kukitambua, mwiko ulioko unawazuia wanajamii kutumia neno hilo hususan katika miktadha ya mijadala ya hadharani. Kwa sababu hiyo, inabidi suala hilo lijadiliwe kwa matumizi ya tasfida ambapo kitendo cha kufanya ngono kilirejelea kama **gosoma egatiba** (kusoma katiba). Mfano wa muktadha wa matumizi wa neno hilo unapatikana katika sehemu yya mazungumzo ifuatayo:

4. **Muktadha:** Mazungumzo haya yalitolewa katika mazungumzo ya ushauri yaliyotokea Katika redio (Egesa Fm) wakati wa kipindi maalum cha ushauri. Mshauri anawataka wanaume kutumia kinga wanapofanya ngono nje ya ndoa.

Msh: Kerabe rende gaki aye buna omosacha tokonyara gwetanga gosoka isiko, koranche tobaise gosoma ekatiba aairia isiko bosa igo... tumia ekondomu.’

Iwapo basi wewe kama mwanaume huwezi kujizuia kutoka nje, tafadhali usisome katiba pale nje bila kitu...tumia kondomu.

Katika tamko hili, mshauri anarejelea kitendo cha kufanya ngono kama kusoma katika. Hii ni kwa sababu kutumia neno la Ekegusii katika kutaja kitendo hicho kungeleta aibu katika mazungumzo hayo. Kwa hivyo, mfano huo wa kutumia **egatiba** kurejelea ngono unakuwa ni utohozi kutokana na tasfida.

Hitimisho

Makala haya yamejadili utohozi unavyotumiwa katika kujadili masuala ambayo ni mwiko katika lugha ya Ekegusii. Utohozi unatumika kutokanana na hali kwamba, lugha ya Ekegusii kama vile lugha nyinginezo imeweka mwiko kwa baadhi ya mambo. Miongoni mwa msuala ambayo ni mwiko kujadiliwa kwa lugha wazi katika lugha hiyo ni pamoja na sehemu za siri, kitendo cha ngono na haja za kibaolojia. Mazungumzo kuhusu VVU na ukimwi hayawezi kukamilika bila kuwepo na mijadala kuhusu sehemu za siri, matumizi ya kondomu na kitendo cha ngono. Makala hayameangazia utohozi ulivyotumika katika mijadla kuhusu sehemu za siri za wanawake na wanaume, kitendo cha ngono na matumizi ya kondomu kama kifaa cha kuzuia maambukizi. Lugha ni sehemu muhimu ya utamaduni wa watu, kwa hivyo utafiti huu ulilenga hasa kuchunguza namna lugha inavyokabiliana na suala ambalo kiasilia halikuwepo katika jamii hii, bali limeibuka miaka kadhaa iliyopita, yaani suala la VVU/ukimwi. Tafiti

nyingine zinazoangazia vipengee mbalimbali vya lugha za Kiafrika zastahili kufanywa kwani lugha hizi ni zetu na ni sharti tuzitafitie.

Marejeleo

- Airhihenbuwa, C. O. na Obergon, R. A. (2000). "Critical Assessment of Theories/models used in Health Communication for HIV/AIDS." *Journal on Health Communication: 5-15*.
- Akama, J.S. na Maxon R. (2006). *The Ethnography of The Gusii of Western Kenya: A Vanishing Cultural Heritage*. Ceredigion, Wales: The Edwin Mullen Press LTD Lampeter.
- Ambasa-Shisanya, C. (2009). *Cultural Determinants of Adoption of HIV/AIDS Prevention Measures and Strategies Among Girls and Women in Western Kenya*. Addis Ababa: OSSREA.
- Baraza ka Liswahili la Taifa (2017). Kamusi Kuu ya Kiswahili. Nairobi, Longhorn.
- Brown, L., na Wenzake. (2001). *Voluntary Counselling and Testing in Sub-Saharan Africa: An Overview*. Washington DC: Horizons/Population Council.
- Cain, D. na Wenzake. (2011). "Language choice and sexual communication among Xhosa speakers in Cape Town, South Africa: implications for HIV prevention message development." *Health Education research Journal XXVI.3: 476-488*.
- Coulmas, F. (2005). *The Study of Speakers Choices*. New York: Cambridge University Press.
- Iwuagwu, S. (2003). "Challenges of Stigma and Discrimination to Voluntary Counselling and Testing (Vcts): communication Implications." Emevwo, B, J. Mathangwane na D Odallo. *The discourse of HIV/AIDS in Africa*. University of Botswana.
- Jones, R. (1996). *Talking AID in Hong Kong: Cultural Models in Public Health Discourse*. Asia, Asia Pacific Media Educator.
- Kiputiputi, O.M. (2011). Kamusi Sanifu ya Kompyuta . Dar Es Salaam, TATAKI
- Kobia, J. (2008). "Metaphors on HIV/AIDS Discourse Among Oluluyia Speakers of Western Kenya." *CADAAD Journal II.2 (2008): 48-66*. 29 September 2017. <http://www.cadaad.net/journal>.
- Moto, F. (2004). "Towards a Study of the Lexicon of Sex and HIV/AIDS." *Nordic Journal of African Studies XIII.3 343-362*.
- Mweri, J.G. (2010). *Utangulizi wa Isimu*. Nairobi. Kenya Literature Bureau,.
- Nurse, D. na G. Phillipson. (1980). "Bantu Languages of East Africa." Polome, E. C. na C. P. Hill. *Language in Tanzania*. London : Oxford University Press.
- Nyakoe, D. G. (2011). "A Semantic Analysis of EkeGusii Euphemism." *Tasnifu ya Uzamili*, Chuo Kikuu cha Maseno.

- Nyandiba, C.N. (2013). "Uchanganuzi wa Mikakati ya Kiisimu ya Mawasiliano katika Diskosi za VVU/Ukimwi Miongoni mwa Abagusii." *Tasnifu ya Uzamifu*, Chuo Kikuu cha Moi
- Ogechi, N. O. (2005). "The Language of Sex and HIV/AIDS among University Students in Kenya." *Stichproben - Vienna Journal of African Studies* V.9 123-149.
- Socrar, P. (2009). "Teaching taboo topics without talking about them: An Epistemic study of a new Approach to HIV/AIDS prevention education in India." *Tasnifu ya Uzamifu*, Chuo Kikuu cha Stanford .
- Veliswa, M. (2009). "Intercultural Communication in Three Eastern Cape HIV/AIDS Clinics." *Tasnifu ya Uzamili*: Chuo Kikuu cha Rhodes.
- Wardhaugh, R. (1999). *Proper English: Myths and Misunderstanding about Language*. Oxford: Blackwell Publishers.